

MATUMIZI YA LUGHA YA VIJANA KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

Faraja Mwendamseke na Saul Bichwa

Ikisiri

Makala hii imejadili matumizi ya lugha ya vijana wa shule za sekondari nchini Tanzania, na mambo yanayosababisha matumizi hayo. Cheshire (1982) na Milroy (1978, 1987) wanaeleza kuwa utofauti wa lugha hutokana na mahusiano yaliyopo katika kundi linalohusika ambapo hutegemea mila, desturi, na kaida ambazo hufanana katika kundi hilo na kufanya kuwapo kwa matumizi tofauti ya lugha katika matamshi, msamiati na tungo. Makala hii imetumia data kutoka uwandani zinazohusu matumizi ya lugha ya vijana wa sekondari wilaya ya Morogoro. Nadharia ya Milroy (1980) inayohusu mitandao ya kijamii imetumika kuchambua data hizo. Makala hii imebaini kuwa vijana wa sekondari wana matamshi, msamiati na tungo wanazozitumia katika mazungumzo yao ambazo hutofautiana na zile za marika mengine. Hali hii husababishwa na haja ya kuwa na usiri au kuficha maana iliyokusudiwa, ucheshi na utani, kuonesha mshikamano na mazoea yaliyojengeka miongoni mwao.

Utangulizi

Makala hii imechunguza matumizi ya lugha ya vijana nchini Tanzania, hususani wanaosoma katika shule za sekondari mkoani Morogoro. Matumizi ya lugha ya vijana ni jambo ambalo limeshughulikiwa na baadhi ya wataalamu. King’ei (2010) anaeleza kuwa vijana, hasa wa marika yanayokaribiana, huweza kutumia lugha kwa njia yao ya kipekee. Mara nyingi vijana wanapokuwa peke yao, huwa na uhuru wa kubuni au kuzua matumizi mapya ya maneno ambayo hupewa maana maalumu. Aidha, Eckert (1989) anadai kuwa lugha ya vijana ni miongoni mwa lugha ambazo si fasaha, hutumiwa na makundi ya vijana wenye umri unaokaribiana na huwa na mahusiano fulani ya karibu kama vile wanafunzi na vijana wa mtaani. Kutokana na ufafanuzi huu, ni dhahiri kuwa vijana huwa na lugha yao wanayoitumia katika uzungumzaji wao kwa malengo tofautitofauti ya kufikisha ujumbe miongoni mwa vijana wenzao.

Waandishi wengine wamechunguza sababu zinazochangia vijana watumie lugha yao, namna tofautitofauti za matumizi ya lugha hiyo, na namna matumizi ya lugha ya vijana yanavyowapa vijana utambulisho wao (King’ei, keshatajwa; Tiffany, 2009; na Wardhaugh, 2010). Aidha, Cheshire (1982) na Mirloy (1987) wanaeleza kuwa matumizi tofautitofauti ya msamiati au tungo kwa vijana hutokana na mahusiano yaliyopo katika kundi husika ambapo hutegemea mila, desturi na kaida ambazo hufanana katika kundi hilo. Naye Hudson (1993) anaeleza kuwa uhusiano

huu unaweza kuwa wa namna mbalimbali, kama vile wa kifamilia, kirafiki, kikazi, na kiutawala. Zaidi ya hao, Marjohan (1988) anaeleza kuwa uhusiano unaweza kuamua namna ya matumizi ya lugha au mtindo wa lugha utakaotumiwa na wahusika wa mazungumzo.

Pamoja na tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu lugha ya vijana, tafiti hizo zilifanywa kwa vijana wa jamii-lugha nyingine. Hakuna utafiti mahususi uliofanywa kuhusu matumizi ya lugha ya vijana wa shule za sekondari wilaya ya Morogoro peke yake. Kwa hivyo, wanajamii wengine ambao sio vijana wa shule za sekondari wilaya ya Morogoro wanakosa kujua matumizi ya lugha ya vijana hao na namna inavyobeba ujumbe wa vijana hao. Hivyo, kulikuwa na haja ya kufanya utafiti wa aina hii ili kujua tofauti hizo na sababu mbalimbali za vijana kupenda kutumia lugha hiyo. Makala hii inafafanua matumizi ya lugha ya vijana wa shule za sekondari wa wilaya ya Morogoro (wenye umri wa miaka kati ya 14 na 18 waliopo kidato cha kwanza hadi cha nne). Kwa kutumia data iliyokusanywa kutoka kwa vijana hawa, tumebainisha sifa mbalimbali za lugha wanayoitumia na kufafanua mambo yanayosababisha vijana wa shule za sekondari wilaya ya Morogoro kutumia lugha hiyo.

Data iliyotumiwa katika makala hii ilikusanywa uwandani mnamo Agosti hadi Septemba 2018. Data hiyo ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na hojaji. Sampuli iliyotoa data za utafiti huu ilipatikana kutokana na mbinu ya usampulishaji nasibu. Watoa taarifa hao ambao walikuwa vijana wanaosoma katika shule za sekondari waliteuliwa kutoka kwenye kata tatu, nazo ni kata ya Mafiga, kata ya Kichangani na kata ya Sabasaba, zilizopo wilaya ya Morogoro nchini Tanzania. Kila kata ilitoa shule moja ya sekondari; na kutoka kila shule, waliteuliwa wanafunzi 20 kwa uwiano sawa wa jinsi. Sampuli ya utafiti ilihusisha vijana 60, ambao walisaidia kupata data ya kutosha.

Makala hii imeanza kwa kueleza utangulizi. Halafu imefuatiwa na nadharia iliyotumiwa kuchambua data zilizokusanywa kwa ajili ya kuchunguza matumizi ya lugha ya vijana wa sekondari. Baada ya hapo tumeelezea dhana ya matamshi, msamiati na tungo za lugha ya vijana wa sekondari. Zaidi ya hayo, sababu za kutumiwa kwake zimeelezwa. Mwisho, tumetoa hitimisho la makala hii.

Nadharia

Makala hii imetumia nadharia ya *mtandao wa kijamii* iliyoasisiwa na Lesley Milroy mwaka 1980, kuchambua data zinazohusu lugha inayotumiwa na vijana nchini Tanzania ili kubainisha sifa zake na kufafanua sababu za kutumiwa. Milroy anaeleza kwamba kila jamiilugha ina muundo wake; hivyo, mitandao ya kijamii huundwa kwa mifumo mbalimbali ya uhusiano wa wanajamiilugha wenyewe.

Muundo wa mtandao mmoja hutofautiana na muundo wa mtandao mwingine kutokana na aina ya uhusiano wa wanajamiilugha wanaounda mtandao huo. Uhusiano huo umegawanyika katika aina nne zifuatazo: uhusiano msingi, uhusiano wa karibu, uhusiano wa kujirudiarudia na uhusiano wa kimpangilio. Misingi iliyotumika kuongoza uchanganuzi wa data ni: (i) washiriki wanaounda mtandao wa kijamii ambao ni vijana wenyewe, na (ii) mahusiano ya vijana ambayo yametokana na ukaribu walionao hatimaye kuweza kuunda jamiilugha yao.

Milroy (keshatajwa) anaeleza kuwa jamiilugha huundwa na mahusiano ya kimtandao wa kijamii unaozingatia kundi dogo kabisa la wanajamiilugha pamoja na kuzingatia aina tofauti za usemaji unaowatofautisha na wazungumzaji wengine wa lugha hiyo. Kwa hiyo, nadharia hii inamaanisha kuwa kuna wazungumzaji wachache wanaohusiana mara kwa mara katika mazungumzo yao na kusababisha kuwapo kwa namna tofauti ya kutumiwa kwa lugha hiyo. Kwa mantiki hiyo, tumechunguza namna mahusiano ya vijana wa shule za sekondari za wilaya ya Morogoro yanavyounda jamiilugha yao na kuwafanya watofautiane na marika mengine.

Nadharia hii ya Milroy inaungwa mkono na Mekacha (2011) na Msanjila na wenzie (2011) wanaoeleza kuwa nadharia hii inatodokezea uwezekano wa kuwapo kwa tofauti za uzungumzaji zinazounda jamiilugha ndogondogo ndani ya jamiilugha moja. Kwa hiyo, nadharia hii imetumiwa kuonesha tofauti zilizopo katika matumizi ya lugha ya vijana wa shule za sekondari za wilaya ya Morogoro, hali inayochombezwa na mahusiano yao yanayounda mitandao ya kijamii. Vipengele vinavyofuata vinafafanua sifa mbalimbali za lugha inayotumiwa na vijana wanaosoma katika shule za sekondari za wilaya ya Morogoro.

Matamshi, Msamiati na Tungo za Lugha ya Vijana wa Sekondari

Uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka kwa vijana wanaosoma katika shule za sekondari za wilaya ya Morogoro ulionesha kuwa lugha wanayoitumia wao kwa wao inazo sifa mahususi zinazohusu matamshi, msamiati, na miundo ya tungo. Tumeeleza vipengele hivi kimoja baada ya kingine, na kuonesha namna matumizi yake yanavyotofautiana na yale ya lugha wanayoitumia pale wanapozungumza na watu wa marika mengine, kama vile walimu au wazazi wao.

Matamshi ya Lugha ya Vijana wa Shule za Sekondari

Uchambuzi wa data za utafiti wetu ulibainisha baadhi ya matamshi ya kipekee yanayotumiwa na vijana wa shule za sekondari katika mazungumzo yao. Mathalani, vijana, hasa wa maeneo ya Sabasaba, Mafiga na Kichangani, husikika wakitamka silabi **-za** mwishoni mwa kila neno. Wakati mwingine, kutokea kwa silabi hiyo

huendana na kudondoshwa kwa silabi fulani katika neno husika, kama inavyooneshwa katika [1] hapa chini:

- [1] (a) Kipaza mmoza aza. = Kipanga mmoja anakuja.
(b) Mwaliza huza mmoza = Mwalimu huyu ‘mnoko’ sana.
saza.
(c) Maza amekuza. = Mama amekuja.

Data hii inaonesha kuwa vijana hao wa shule za sekondari hupendelea kubadili silabi ya/za mwisho ya/za maneno wanayoyatumia katika mazungumzo yao. Hali hiyo husababisha kubadili maumbo yake halisi ingawa maana inayokusudiwa ya tungo husika hubaki kuwa ileile. Namna hii ya utamkaji huwatofautisha wazungumzaji hawa na wazungumzaji wa marika mengine. Sababu mojawapo inayoelekea kuibua utamkaji wa namna hii ni ubunifu wa vijana wa shule za sekondari wakilenga kuipamba lugha yao. Namna hii ya utamkaji hutumiwa na vijana hao pale wanapowasiliana wao kwa wao; lakini wanapokuwa na walimu wao, hubadili namna ya utamkaji wao kama inavyooneshwa katika [2] hapa chini:

- [2] Mwanafunzi: Samahani, mwalimu, mama amekuja.
Mwalimu: Amekuja saa ngapi?
Mwanafunzi: Amekuja sasa hivi.

Kama mfano [2] unavyoonesha, mwanafunzi huyu anazungumza na mwalimu wake pasipo kubadili matamshi ya maneno. Laiti angekuwa anazungumza na wanarika wenzake, tungetarajia kumsikia akitamka: *Samahaza, mwaliza, maza amekuza*. Badala yake, anazungumza Kiswahili fasaha kwa sababu uhusiano uliopo kati yake na mwalimu wake ni tofauti na anavyohusiana na wanafunzi wenzake. Hoja hii inaelezwa pia na Cheshire (1982) na Eckert (1989) kuwa lugha ya vijana ni miongoni mwa lugha ambazo si fasaha, ambapo huweza kubadili hata matamshi sahihi katika mazungumzo yao kwa ajili ya kuelewana wao wenyewe.

Msamiati wa Lugha ya Vijana wa Shule za Sekondari

Msamiati ni sifa nyingine ya pekee ya lugha inayotumiwa na vijana wa shule za sekondari wa wilaya ya Morogoro inahusu msamiati wake. Msamiati wa lugha ya vijana wa shule za sekondari huweza kujibainisha kwa kuchanganya msamiati wa lugha mbili tofauti. Utumiaji wa kuchanganya msamiati husababishwa na jamiilugha yao kuwa na matumizi ya lugha zaidi ya moja. Ijapokuwa dhana hii pia hujidhihirisha kwa marika mengine, lakini data ilionesha kuwa wanaitumia kwa kiasi kikubwa ili kutambulisha usomi wao. Licha ya matumizi ya msamiati huo, kuna wakati mwingine hutumia msamiati wa kubuni ili kuweza kuwasiliana wao kwa wao. Matumizi ya msamiati huo yanajibainisha kama ifuatavyo:

Uchanganyaji wa Msamiati wa Lugha Mbili Tofauti

Msamiati wa lugha ya vijana wa shule za sekondari unaotokana na kuchanganya msamiati wa lugha mbalimbali husababishwa na kuwapo kwa wingilugha. Pia, hali hiyo huchangiwa na utandawazi unaopatikana sana katika mitandao ya kijamii, kama vile *Facebook*, *Twitter*, *WhatsApp*, na *Instagram*, na katika jumbe za simu za mkononi. Katika mitandao hii ya kijamii kuna matumizi mengi ya uchanganyaji msimbo kunakochangia watumiaji wa mitandao hiyo kuanza kutumia katika mazungumzo ya kawaida. Mfano [3] hapa chini unaonesha hivyo.

- [3] (a) *Juma amemblock mwalimu.* = Juma hamsikilizi mwalimu.
(b) Demu yule *anamute* sana. = Msichana yule hatongozeki.
(c) Mtoto wa *dog-kuu* leo = Mtoto anayefungiwa ndani leo kaachiwa.

Msamiati huu unatokana na lugha mbili, yaani Kiingereza na Kiswahili. Katika [3a], msamiati <amemblock> umetokana na neno la Kiingereza <block> ‘kizuizi’ lililoambikwa kiambishi cha Kiswahili {a-} na {-me-} mwanzoni. Katika [3b], msamiati <anamute> umetokana na neno la Kiingereza <mute> ‘kimya’ lililoambikwa viambishi awali vya Kiswahili {a-} na {na-}. Katika [3c], msamiati <dog-kuu> umetokana na uambatishaji wa neno la Kiingereza <dog> ‘mbwa’ na neno la Kiswahili <kuu>.

Mwelekeo huu wa kuunda maneno kwa kuchanganya maneno ya lugha mbili (au zaidi) hautumiwi katika lugha ya vijana wanaosoma katika shule za sekondari za wilaya ya Morogoro pekee. Mathalani, King’ei (keshatajwa) anaeleza kuwa mfumo wa mawasiliano ya lugha ya Sheng ambayo hutumiwa hasa na vijana nao una maneno yaliyotokana na lugha mbili au zaidi.

Msamiati wa Kubuni

Vijana wa shule za sekondari huweza kubuni msamiati katika mazungumzo yao kutokana na mawazo mapya ya vitu vipya vinavyojitokeza kila siku. Pia, huweza kubuni msamiati mwingine ulio tofauti na maneno mengine waliyokuwa wakiyatumia kama wakiona msamiati wao umeshazoeleka na kufahamika na watumiaji wengine wa jamii. Hivyo, msamiati wao una sifa ya kuibuka na kutoweka baada ya kutumiwa kwa muda fulani.

Maneno kama <kuanuka>, <kuchikichia> au <kusele> hutumiwa yakimaanisha ‘kuondoka au kutoroka darasani au shuleni’. Msamiati huu hutumiwa katika mazingira ya shuleni ili kuwatenga watu wengine, kama vile walimu, wasielewe yale wanayoyafanya ambayo si mazuri, kama vile kutoroka shule na kwenda mtaani kuzurura au kuvuta bangi.

Hata hivyo, wanafunzi hawa wanapotaka kuzungumza na walimu wao, hawatatumia msamiati huu wa kubuni, kama vile <kuanuka>, <kuchikichia> au <kusele> kwa kuwa hawatakuwa na lengo la kuficha/kutunza siri fulani. Mathalani, badala ya kutumia msamiati huo, mwanafunzi akitaka kuondoka darasani, ataomba ruhusa kwa mwalimu wake kwa kutumia msamiati uliozoeleka, *akisema: Samahani, mwalimu, ninaomba ruhusa niende nyumbani; ninajisikia vibaya.*

Miundo ya Tungo za Lugha ya Vijana wa Shule za Sekondari

Uchunguzi wa data iliyokusanywa ulionesha kuwa tungo zinazotumiwa na vijana wa shule za sekondari wa wilaya ya Morogoro katika mazungumzo yao huwa zina sifa zifuatazo:

Huwa Fupifupi

Tungo za vijana wa shule za sekondari huelekea kuwa na maneno machache, kama Mfano [4] unavyoonesha:

- | | | | |
|---------|------------------|---|--------------------|
| [4] (a) | Dingi noma. | = | Baba mkali. |
| (b) | Tupotee fasta. | = | Tuondoke haraka. |
| (c) | Tulizana kwanza. | = | Nyamaza. |
| (d) | Kidoti kaja. | = | Mchonganishi kaja. |

Mara nyingi vijana wa shule za sekondari hutumia tungo fupifupi kwa lengo la kupeana taarifa au ishara kuhusu jambo wanalotaka kulifanya ili lisieleweke kwa watu wengine. Hata hivyo, wanapozungumza na walimu au wazazi wao, hali huwa tofauti kwani hutumia tungo ndefu. Inavyoelekea, vijana hawa huepuka kutumia tungo fupifupi kwa kuchelea kutoeleweka kwa walimu au wazazi wao.

Huchanganya Msimbo katika Tungo

Mazungumzo ya vijana hawa wa shule za sekondari huweza kutumia sentensi nyingi zilizochanganya maneno ya lugha mbili tofauti, hususani, maneno ya Kiswahili na Kiingereza. Mfano [5] unaonesha na kufafanua jinsi sentensi za lugha ya vijana wa Morogoro zinavyochanganya maneno ya lugha mbili tofauti:

- | | | | |
|---------|--|---|-------------------------------|
| [5] (a) | Tomorrow tutaibuka first | = | Kesho tutakuwa wa kwanza. |
| | first. | | |
| (b) | ‘Mademu’ wa class vimeo. | = | Wasichana wa darasani malaya. |
| (c) | M-look madam. | = | Mwangelie mwalimu wa kike. |

Wanafunzi hawa watakapokuwa wanazungumza na walimu wao hawawezi kuchanganya msimbo na kutumia tungo kama: <‘Mademu’ wa **class** vimeo.> au

<M-look madam>. Badala yake, wanatarajiwa kutumia tungo fasaha, kama zilivyobainishwa katika [5].

Inavyoelekea, vijana hawa huchanganya msimbo ili watambulike kuwa wao ni wasomi, au ni vijana wa kisasa wanaokwenda na wakati. Zaidi ya hayo, Coupland na Jaworski (2008) na Grosjean (2010) wanaeleza kuwa kuchanganya msimbo kwa kutumia lugha mbili au zaidi hulenga kuwabagua watu wengine wasijue kinachozungumzwa.

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa lugha ya vijana wa shule za sekondari ina utofauti katika matamshi, msamiati na miundo ya tungo inayotumiwa katika mazungumzo yao. Vijana hawa hufanya hivyo ili kujenga mahusiano yao na kuwatofautisha na wazungumzaji wa makundi mengine. Hali hii inathibitisha wazo la Milroy (1980) katika nadharia yake ya mtandao wa kijamii kuwa mahusiano miongoni mwa wazungumzaji hupelekea kujengeka kwa tofauti ya lugha wanayoitumia katika mazungumzo yao na ile inayotumiwa na wazungumzaji wengine wa lugha hiyo.

Sababu za Vijana wa Sekondari Kutumia Lugha Yao

Lengo la pili la makala hii lilikuwa kuelezea sababu zinazowafanya vijana wa shule za sekondari wapende kutumia lugha yao kwa namna ya pekee. Uchambuzi wa data zilizokusanywa unaonesha kuwa kuna mambo kadha yanayochombeza kutumiwa kwa lugha ya vijana. Vipengele vinavyofuata vinatalii mambo hayo.

Kuficha Maana Iliyoku sudiwa

Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa sababu kuu ya kutumiwa kwa lugha ya vijana ni kuficha maana wanayoikusudia ili isieleweke kwa wale wanaowazunguka kama vile walimu, viongozi wa shule au wazazi wao. Hali hii hutokea pale ambapo mada wanayozungumzia huwa kinyume na sheria, tamaduni au kaida za jamii zinazowazunguka, kama vile kutoroka shule, kufanya fujo, kufanya ngono, kuvuta bangi, kumteta mtu, na hata kukataa kufanya kazi walizopewa wafanye.

Mifano ya maneno yanayotumiwa na vijana hawa wanapotaka kufanya fujo shuleni ni <zali>, <mbinue> au <mwisho leo>. Msamiati huu unapotumiwa, hutoa ishara ya kuanzisha mgomo, wakilenga kufanya chochote almradi matakwa yao yatimie.

Vijana wanapotaka kuzungumzia suala la utoro shuleni, msamiati kama vile <muti>, <dogi> na <mkwanja> hutumiwa. Msamiati huu unapotumiwa na vijana, hulenga kutoa ishara ya kutoroka darasani, wakimaanisha kuwa muda wa kuondoka shuleni waliokusudia wao umewadia. Ama kuhusu masuala ya kufanya ngono, utungo kama vile <Usinitanie unataka machupa sio> hutumiwa. Utungo huu

humaanisha mvulana kumtahadharisha msichana aache kumtania la sivyo atamfanya ngono.

Vijana wa shule za sekondari wanapotumia lugha kwa namna hii, watu wanaowazunguka, kama vile walimu, hushindwa kuelewa maana ya kile kinachozungumzwa hata kama watawasikiliza mazungumzo yao. Matokeo yake, vijana hawa huendelea kufanya mambo yao kwa siri. Sababu hii inaungwa mkono na King’ei (keshatajwa), ambaye anaeleza kuwa vijana wanapokuwa katika mazungumzo yao, hutumia lugha kwa namna ya pekee kwa lengo la kuficha maana iliyokusudiwa ili isieleweke kwa wale wanaowazunguka.

Kuleta Ucheshi na Utani

Vijana wa shule za sekondari wanapokuwa katika mazingira tofauti na ya darasani, kama vile nje ya darasa, sehemu za kula, njiani au katika michezo, hupenda kutaniana na kuchekeshana kutokana na matukio mbalimbali wanayokutana nayo. Lengo huwa ni kuburudika na kupoteza wakati hasa pale wanapokuwa hawana shughuli maalumu ya kufanya. Mathalani, wakiwa wenyewe, hutaniana wao kwa wao au huwatania watu wengine wanaokuwa nao, kama vile wazazi wao na walimu wao. Waweza kutania kuhusu namna mwalimu anavyozungumza, anavyofundisha na hata wao wenyewe wanavyoshindwa kujibu maswali darasani.

Kuonesha Mshikamano Miongoni Mwao

Vijana wa shule za sekondari za wilaya ya Morogoro wanapokuwa wanazungumza kwa namna yao huwafanya vijana wenzao kuwasikiliza, kuwakubali na kuwatambua kuwa wanaozungumza ni vijana wenzao. Kwa hiyo, huendelea kuzungumza nao bila wasiwasi wowote, wakiwashirikisha mambo yahasuyo vijana, kama vile kuficha siri zao. Kama tulivyoeleza katika §4.1.1 hapo awali, hali hii ya kusikilizana na kukubaliana huwajengea umoja na mshikamano miongoni mwao. Mathalani, wakitaka kumgomea mwalimu au uongozi wa shule ili matakwa yao yatimizwe, huwa na lugha wanayoitumia.

Kudhihirisha Mazoea

Vijana wa sekondari hutumia lugha tofauti kutokana na mazoea yao yaliyojengeka katika mazingira wanayokutania; hivyo basi, hujikuta wakitumia lugha hii kila wakati. Hali hii hudhihirika kila mara wanapokutana kwa sababu huzungumza lugha yao. Huizoea lugha hiyo na kuona kuwa ni lugha wanayoweza kuitumia kila mara. Hata kama hakuna watu wengine karibu wanaosikia mazungumzo yao, huendelea kuzungumza lugha hiyo.

Kwa jumla, utafiti umebaini kuwa vijana wa shule za sekondari huwa na mambo mbalimbali yanayosababisha watumie matamshi, msamiati na tungo tofautitofauti katika mazungumzo yao. Hali hiyo huwatofautisha na watu wa marika mengine katika jamii. Hii inatokana na mahusiano waliyokuwa nayo; kama asemavyo Milroy (1980) katika nadharia ya mitandao ya kijamii kuwa uhusiano wa karibu katika jamii hutengeneza jamiilugha yao ili waweze kuwasiliana. Hoja hii inaungwa mkono pia na Marjohan (1988) kwa kueleza namna uhusiano unavyoweza kuamua namna ya matumizi ya lugha au mtindo wa lugha utakaotumiwa na wahusika wa mazungumzo.

Hitimisho

Makala hii imefafanua namna tofautitofauti za matumizi ya lugha ya vijana wa shule za sekondari za wilaya ya Morogoro nchini Tanzania na mambo yanayochombeza kutokea kwa namna hizo za matumizi ya lugha. Uchambuzi wa data iliyotumiwa umedhihirisha kuwa vijana wa wilaya ya Morogoro wana matamshi, msamiati na tungo wanazozitumia katika mazungumzo yao. Pia, kuna mambo kadha wa kadha yanayochangia vijana hawa kutumia lugha kwa namna tofauti kulinganisha na watu wa makundi mengine katika jamii.

Uchunguzi umeonyesha kuwa aina hii ya matumizi ya lugha haihusu vijana wa wilaya ya Morogoro pekee, bali vijana wa rika hilo katika maeneo mbalimbali duniani nao wana namna zao za kuwasiliana na vijana wengine wa rika lao katika jamii zao. Makala imedhihirisha misingi ya nadharia ya mtandao wa kijamii ya Milroy (1980) kwa kuonesha kuwa vijana huunda mtandao wao kutokana na mahusiano yao kutegemea mila, desturi na kaida zinazofanana katika kundi hilo na kusababisha kuwapo kwa matumizi tofauti ya lugha katika jamiilugha yao na kutofautiana na watu wa marika mengine. Makala hii inapendekeza kuwa utafiti ufanyike katika marika mengine, kama vile wazee na watoto, ili kubaini tofauti za matumizi ya lugha inayotumiwa na watu wa marika hayo. Utafiti huo utasaidia kubaini ni kwa namna gani marika ya wazee na watoto huunda mitandao yao ya kijamii kutokana na mahusiano yao.

Marejeleo

- Cheshire, J (1982). *Variation in an English Dialect*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Coupland, N. and Jaworski, A. (2008). *Sociolinguistics: A Reader and Coursebook*. Pelgrave: Routledge.
- Eckert, P. (1989). *Jockes and Burnouts: Social Categories and Identity in the High School*. Cambridge: Teachers' College Press.

- Grosjean, F. (2010). *Bilingual: Life and Reality*. Harvard: Mass Harvard University Press.
- Hudson, R. A. (1993). *Sociolinguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- King'ei, K. (2010). *Isimujamii. Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Marjohan, A (1988). *An Introduction to Sociolinguistics*. Jakarta: Proyek Pengembangan Lembaga Pendidikan Tenaga Kependidikan, Dikti, Depdikbud.
- Mekacha, R. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Mukhadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.
- Milroy, L. (1978). "Belfast: Change and Variation in an Urban Vernacular." *Sociolinguistic Patterns in British English*, edited by P. Trudgill, Arnold, pp. 19–36.
- _____ (1980). *Language and Social Networks*. Basil: Blackwell
- _____ (1987). *Language and Social Networks*. Basil: Blackwell.
- Msanjila, Y. P, Kihore, Y. M. & Massamba D. P. B. (2011). *Isimujamii: Sekondari Na Vyuu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Tiffany, S. L. (2009). "Language, Identity and Power: Navajo and Pueblo Young Adults Perspectives and Experiences with Competing Language Ideologies." *Journal of Language, Identity & Education*, vol. 8, no. 2, pp. 307–10.
- Wardhaugh, R. (2010). *An Introduction to Sociolinguistics*. Basil: Blackwell.